TANGAZO LA SERIKALI NA………...la tarehe …………...

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)**

**(SURA YA 287)**

---

**SHERIA NDOGO**
**Zimetungwa chini ya kifungu cha 153**

# SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA (MAHUDHURIO YA LAZIMA NA UPATIKANAJI WA CHAKULA CHA MCHANA MASHULENI) ZA MWAKA 2023

*Jina la sheria na tarehe ya kuanza kutumika*

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za Halmashauri ya Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba (*Mahudhurio ya Lazima na Upatikanaji wa Chakula cha Mchana Mashuleni*) za mwaka 2023 na zitatumika ndani ya eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba na zitaanza kutumika kuanzia tarehe zitakapotangazwa katika Gazeti la Serikali.

*Tafsiri*

2. Katika Sheria Ndogo hizi, neno:

   "**Chakula**" maana yake ni chakula cha mchana kinachotolewa shuleni

   "**Halmashauri**" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba;

   "**Shule**" maana yake ni shule zote za serikali za awali, msingi na sekondari zilizomo ndani ya eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba;

   "**Mzazi**" maana yake ni baba au mama wa mtoto aliyeandikishwa shuleni;

   "**Mlezi**" maana yake ni mtu yeyote aliyekabidhiwa jukumu la kumlea mtoto aliyeandikishwa shuleni;

   "**Serikali ya Mtaa**" maana yake ni Halmashauri ya Kijiji ambako wanatoka wanafunzi wanaosoma katika shule husika ya msingi na sekondari.

   "**Sheria**" maana yake ni Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba (Mahudhurio ya lazima na Upatikanaji wa Chakula cha Mchana Mashuleni)

   "**Umri wa kwenda Shule**" maana yake ni umri mtoto kati ya miaka mitano mpaka sita kwa elimu ya awali, miaka sita hadi saba kwa darasa la kwanza na sekondari ni umri baada ya kumaliza darasa la saba.

*Kuandikishwa na Mahudhurio*

3. Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kila mzazi au mlezi atahakikisha kuwa mtoto wake mwenye umri wa kwenda shule anaandikishwa na kupelekwa shuleni ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa anahudhuria masomo kwenye shule hiyo kwa lazima, katika siku zote za masomo na siku zingine zozote zisizokuwa za masomo na atakazotakiwa kuhudhuria shuleni, mpaka atakapomaliza Elimu ya Msingi na Sekondari.

4. (1) Mara baada ya kuandikishwa shule, kila mtoto mwenye umri wa kwenda shule atahakikisha kuwa anahudhuria masomo kwenye shule aliyoandikishwa katika kila siku ambayo atatakiwa kufika shuleni kwaajili ya masomo na ama siku zingine zozote ambazo sio za masomo lakini atakapohitajika kuwepo shuleni.

*Wajibu wa kila mwanafunzi kuhudhuria shuleni*

(2) Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kwa mwanafunzi aliyeandikishwa, kutohudhuria shuleni bila sababu zozote za msingi na kwamba endapo itabainika kuwa mwanfunzi huyo ahajahudhuria masomo shuleni katika siku za masomo, pamoja na kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria za shule, atapewa adhabu kali ikiwa ni pamoja na kutakiwa kurejea shuleni kwaajili ya kuendelea na masomo mpaka pale ambapo atamaliza elimu yake.

(3) Endapo itabainika kuwa mwanafunzi aliyendikishwa ameshindwa kuhudhuria masomo yake kutokana na sababu za msingi, mzazi au mlezi wa mtoto huyo atakuwa na jukumu la kufikisha shuleni taarifa za mtoto wake zilizopelekea kushindwa kuhudhuria masomo yake katika siku na wakati aliotakiwa kuhudhuria shuleni na endapo mzazi au mlezi atashindwa kufanya hivyo, atahesabika kuwa hajatekeleza wajibu wake na atastahili kupatiwa adhabu kama ya mzazi au mlezi aliyeshindwa kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

5. (1) Mzazi au mlezi atachangia debe mbili za mahindi, nusu debe la maharage au fedha sawa na bei ya sokoni pamoja na mchango wa Sh. 20,000/= kwa kila mwanafunzi kwa mwaka kama mchango wa chakula cha mchana kwa ajili ya kumuwezesha mtoto wake kupata chakula cha mchana shuleni.

*Mchango wa chakula cha mchana*

(2) Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria hizi, kwa mzazi au mlezi kwa kutokujali au kukataa kushindwa kuchangia mchango wa chakula cha mchana kwaajili ya mtoto wake.

6. (1) Halmashauri haitawasamehe wazazi ama walezi wasio na uwezo wa kulipa michango ya chakula inayohitajika shulenis, isipokuwa kwamba Serikali za Vijiji, kwa kushirikiana na Kamati ya Maendeleo ya Kata husika, zitawalipia michango ya chakula watoto ambao wazazi au walezi wao watathibitika kutokuwa na uwezo wa kulipa michango hiyo.

*Wajibu wa Serikali ya Kijiji na Kamati ya Maendeleo ya Kata*

(2) Serikali ya kijiji itawajibika kumlipia michango katika shule za Msingi na Sekondari kwa mtoto au watoto ambao wazazi au walezi wao watathibitika kutokuwa na uwezo wa kuchanga michango hiyo kabisa.

(3) Bila kuathiri kifungu cha 5(1) na (2) cha Sheria hizi, Serikali ya Kijiji inaweza kuandaa utaratibu wa kubaini wazazi wasiokuwa na uwezo wa kuchangia michango ya gharama za chakula mashuleni kwa watoto wao, na utaratibu huo sharti uidhinishwe na mikutano Mkuu wa Kijiji.

7. Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi itakuwa ni kosa kwa Serikali yoyote ya Kijiji;-
   a) Kushindwa kusimamia uendeshaji wa shule iliyopo ndani ya eneo la Halmashauri yake
   b) Kushindwa kwa kutojali au kukataa kumlipia mtoto michango inayodaiwa katika shule za msingi au sekondari, wakati ambapo imethibitika mzazi au mlezi wa mtoto huyo hana uwezo wa kulipa.
   c) Kushindwa kuzisimamia ipasavyo Kamati za Shule zitakazotoa maamuzi na maelekekezo ya kusimamishwa masomo kwa wanafunzi ambao wazazi wao wameshindwa kulipia michango cha chakula.

8. Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, mzazi au mlezi atakuwa ametenda kosa iwapo:
   a) Atashindwa, hatojali au kukataa kumchangia mtoto gharama za chakula cha mchana Shuleni
   b) kumkataza mtoto kwenda shule au kuendelea kuhudhuria masomo kila siku au kufanya kitendo ambacho kinaathiri uwezekano wa mtoto huyo kuhudhuria shuleni kila siku kwa kigezo cha kukosa ama kushindwa kuchangia chakula shuleni.

*Utaratibu wa kushirikisha wadau kuchangia chakula mashuleni.*

9. (1) Katika kutekeleza Mpango wa Upatikanaji wa chakula mashuleni, Halmashauri itawashirikisha wadau katika:-

   a) Uchangiaji wa moja kwa moja kwa njia ya fedha au misaada kwa ajili ya kuimarisha mpango wa upatikaji wa chakula cha mchana mashuleni;
   b) Kushiriki katika utekelezaji wa mpango wa uchangiaji chakula kwa watoto ambao wazazi au walezi wao hawana uwezo wa kuchangia chakula na ambao wamethibitishwa na uongozi wa serikali.

(2) Mtu yeyote ambaye atahitaji kuchangia michango moja kwa moja kwenye shule sharti azingatie yafuatayo;-

   a) kwa yeyote ambaye atahitaji kuchangia kwa njia ya fedha, atahakikisha kuwa fedha hizo anaziingiza kwenye akaunti ya shule na kuwasilisha hati ya malipo (*bank pay slip*) shuleni hapo, na

   b) kwa yeyote ambaye atahitaji kuchangia kwa njia ya kupeleka chakula shuleni, atahakikisha kuwa anapeleka chakula kisichopikwa kama vile mahindi, mchele, maharage, kunde, mbaazi, choroko, njugu kwa kuvikabidhi kwa mkuu wa shule husika.

   c) Kwa minajili ya Sheria Ndogo hizi, itakuwa ni marufuku kwa mtu, watu au taasisi yoyote ile kupeleka shuleni mchango wa chakula

kilichopikwa, ili kulinda usalama wa afya za wanafunzi.

## MAKOSA NA ADHABU

*Makosa na adhabu*

10 Ikiwa mtu yeyote:-

(a) Atadharau, atabeza au kwa makusudi atakaidi kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na Mpango wa uchangiaji wa chakula cha mchana mashuleni chini ya kifungu cha 4(2), 6 na 7 Sheria Ndogo hizi;

(b) Atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kushiriki kutekeleza Mpango wa uchangiaji chakula cha mchana shuleni;

(c) Atatoa kwa makusudi huku akijua ni kosa taarifa za uongo kwa Halmashauri;

(d) Atashindwa kutoa taarifa zitakazohitajika na Halmashauri;

(e) Atamzuia Afisa Muidhiniwa kutekeleza majukumu yake;

Atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000) au kutumikia kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili (12) jela au adhabu zote mbili yaani faini na kifungo kwa pamoja.

*Kufifilisha kosa*

11. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyopungua shilingi Laki Mbili tu (200,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kulipa faini iliyoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi.

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ilibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa azimio lililopitishwa na Halmashauri katika kikao kilichoketi na kufanyika tarehe……………………… na ilibandikwa mbele ya:

…..………………………………

**MARIAM SAID MWANZALIMA**

*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba*

…………………………………

**BAISA ABDALLAH BAISA**

*Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba*

**NAKUBALI**

**…………………………………………………….**

**ANGELLAH JASMINE KAIRUKI (MB)**
**WAZIRI WA NCHI – OFISI YA RAIS**
**(TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITA)**

**Dodoma,**
**Julai, 2023**